MAONI & UCHAMBUZI

"Uuguzi ni sanaa, na kama ni sanaa, inahitaji kujitoa kwa hali ya juu, kama maandalizi ya mchoraji au mfinyanzi,"

Florence Nightingales

MWANANCHI

Dar es Salaam, Ijumaa, Novemba 4, 2016

Uharaka wa Muswada wa Habari unatia shaka

Septemba 16, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Nape Nnauye alisoma kwa mara ya kwanza bungeni muswada wa Sheria ya Huduma za Habari wa mwaka 2016.

Kusomwa kwa muswada huu, kulimaanisha kuanza kwa shughuli muhimu ya wadau kuupitia kwa maana ya kusoma, kuchambua na kutoa mapendekezo.

Hata hivyo, kabla na hata baada ya muswada huo kusomwa bungeni, wadau wa vyombo vya habari wamekuwa mstari wa mbele kuukosoa kwa kuwa na maeneo kadhaa ya upungufu yanayohitaji maoni ya kina ya wadau.

Ni ukweli usiopingika kuwa kwa muda mrefu, Serikali na wanahabari wamekuwa na kiu ya kuwa na sheria itakayowasimamia kama wanataaluma; itakayowalinda na kutambua hadhi ya taalamu yao kama ilivyo taaluma nyingine.

Lakini, tunajiuliza kwa nini mchakato wake unaharakishwa, kwa nini wadau hasa wanahabari hatupewi nafasi ya kutosha ya kutoa maoni ya kina kama ilivyofanyika kwa wanasheria waliousoma na kuchambua kisheria?

Kilio kikuu chetu kama wanahabari ni kuwapo kwa vifungu kadhaa tunavyoamini havina dhamira njema na wanahabari, vyombo vya habari na taaluma kwa jumla.

Vifungu hivyo ni pamoja na kile cha 55 kinachompa waziri husika mamlaka ya kufuta chombo chochote cha habari hata kama amesukumwa kufanya hivyo kwa utashi binafsi. Pia, kifungu cha 60 (a), kinampa uwezo waziri kutunga kanuni za utoaji wa taarifa za mapato kwa vyombo vya habari hata vile binafsi.

Aidha, ukiondoa faini na adhabu za gerezani, kifungu cha 13 (a) kinaeleza kuwa mwandishi akifanya kosa hata kwa bahati mbaya, anaweza kuondolewa kwenye orodha ya wanahabari na kuzuiwa kabisa kufanya kazi katika sekta ya habari au taaluma inayohusiana na habari.

Haya ni baadhi tu ya mambo yanayotutatiza wanahabari na kimsingi tunakwazika zaidi hasa tunapoona baadhi ya watu wakitaka kuuburuza mchakato.

Sheria inayotaka kutungwa mbali ya kasoro hizo tulizotaja hapo juu, ina mambo mengi ambayo kwa mtazamo wetu kama wadau wakuu hayahitaji uharaka, ndiyo maana kupitia vyombo vyetu vya kitaaluma, tumeomba tupewe muda hadi Februari mwakani kwa ajili ya kuupitia muswada na kutoa maoni yatakayojali masilahi ya pande zote.

Tunakiri kuwa siyo kazi yetu kuingilia mchakato wa utunzi wa sheria wala kuzuia utekelezaji wake, tunachoisihi Serikali ni kutupa fursa ya kuujadili muswada kwa mapana yake, hasa kwa kuzingatia kuwa sheria hii imekuwa ikipiganiwa kwa miongo kadhaa.

Tunachohitaji ni kuwa na sheria itakayolinda maslahi ya taaluma, wanahabari na nchi yetu kwa jumla.

Kilichopo sasa ni sheria inayoonekana kujaa vifungu vinavyobeba dhana ya vitisho, kukomoana na kuleta hofu badala ya matumaini kwa wahusika.

Ili tusifike hatua ya kuwa na sheria nyingine yenye vipengele kandamizi kama ilivyo kwa sheria ya sasa, tunaisihi Serikali yetu ambayo moja ya sifa zake adhimu ni kuwa sikivu, ione haja ya kutupa nafasi ya kuupitia muswada kwa kina ili hatimaye Taifa lipate sheria bora kwa ustawi wa taaluma, wanahabari na maendeleo ya nchi kwa jumla.

KIPANYA

HUTOLEWA NA MWANANCHI COMMUNICATIONS LTD

Barabara ya Mandela, SLP 19754, Dar es Salaam.
+255 22 24 50875, 0754 780647
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Francis Nanai: Mkurugenzi Mtendaji
Bakari Machumu: Mhariri Mtendaji Mkuu
Frank Sanga: Mhariri Mtendaji

AIDAN EYAKUZE

Muswada wa Habari ni kitanzi kwa demokrasia

Mwaka 1801, miaka 25 baada ya Marekani kupata Uhuru kutoka kwa Uingereza, Thomas Jefferson alitawazwa kuwa rais wa tatu wa nchi hiyo. Magazeti yalimshambulia ila alipambana nayo. "Nalaani uozo unaoenezwa na magazeti. Tumefika mahali hatuwezi kuamini kinachoandikwa magazetini," alisema na kuongeza: "Pamoja na hayo, Jefferson aliamini kuna umuhimu wa vyombo vya habari imara na huru. "Kama ningetakiwa kuchagua iwapo tuwe na Serikali bila magazeti ama magazeti bila Serikali, basi nisingesita hata kidogo kuchagua magazeti bila Serikali."

Ni jambo la kawaida kabisa kwa viongozi wa Serikali kuchukia vyombo vya habari. Katika jambo hili, viongozi wetu na wale wa nchi nyingine duniani wanakubaliana. Na zama hizi zinafanana na zile Marekani, mwaka 1800.

Lakini, mtazamo wa Rais Jefferson ni kwamba bila kuwa na vyombo vya habari imara na huru, hakutakuwa na uwajibikaji. Na bila kuwajibishwa, Serikali haitafanya kazi kwa maslahi ya nchi wala wananchi wake.

Tanzania, Sheria ya Magazeti (1976) ndiyo mama inayoongoza utendaji wa magazeti. Sheria hii imekuwa ikilalamikiwa kwa muda mrefu kwa kumpa waziri mamlaka ya kuyafungia bila taarifa ama kukata rufaa. Sheria hii inatumika na mwaka huu pekee, vyombo vinne vya habari vimefugiwa.

Mwaka 1992, Tume ya Jaji Nyalali, iliyopendekeza mfumo wa demokrasia ya vyama vingi, ilieleza Sheria hiyo inakuika Katiba ya Jamhuri ya Muungano hivyo ilipaswa kurekebishwa au kufutwa ili kulinda uhuru wa vyombo vya habari.

Tume ya Nyalali ilitambua umuhimu wa uhuru wa vyombo vya habari katika kustawisha demokrasia na maendeleo ya nchi. Vyombo huru vya habari hufuatilia kazi zinazofanywa na Serikali na wananchi kuchangia maoni yao kwenye masuala ya jamii na taifa letu.

Muswada huu wa Habari ambao unajadiliwa bungeni ni fursa nzuri ya kuainisha matatizo yaliyopo ili sekta ya habari iweze kwenda na wakati kwa kuzingatia Katiba ya nchi pamoja na sheria za kimataifa.

Kwa bahati mbaya kwa namna ulivyo sasa, muswada huu utadhoofisha uhuru wa vyombo vya habari. Kuupitisha huu bila kufanyia marekebisho ya msingi ni hatua ya kuhatarisha demokrasia yetu changa.

Kwanza, unaipa Serikali mamlaka ya kuwabana waandishi kwa kuanzisha mfumo wa kupata vibali, kupitia Bodi ya Ithibati ya Wanahabari ambayo itakuwa na wajumbe saba. Wote watateuliwa na Waziri.

Sheria na taratibu za kimataifa zinasema si halali kutoa vibali kwa waandishi wa habari ama kuweka masharti ya anayeweza kuwa mwandishi wa habari. Muswada huu ukipitishwa, waandishi wote nchini watakuwa na hofu ya kunyang'anywa vibali vyao.

1992, Tume ya Jaji Nyalali, iliieleza Sheria Magazeti ya mwaka 1976 inakuika Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Pili, unataka vyombo vya habari (magazeti) kuwa na leseni. Unaipa Serikali mamlaka ya kusimamia utoaji wa leseni hizo. Tatizo kuu la Sheria ya Magazeti (1976) litaendelea kubaki palepale.

Tatu, muswada unaingilia uhuru wa vyombo vya habari vikiwamo binafsi, kwa kuweka uwezekano wa kuvilazimisha, kutangaza habari kama inavyoelekezwa na Serikali.

Nne, vifungu vinavyohusu kashfa na uchochezi vinavuka mipaka inayokubalika kidemokrasia. Kwa mfano, kuna kifungu kinasema kauli iliyochapishwa inaweza kuwa kashfa hata kama ni ya ukweli. Unaainisha kauli ni lazima iwe ya kweli na "yenye manufaa kwa umma". Bila shaka Serikali ndiyo itakayoamua kauli ipi "ina manufaa kwa umma."

Hakuna anayesema vyombo vya habari nchini vimekamilika. Bado vinaandamwa na upendeleo, rushwa na uongo. Ukipita kama ulivyo, utanyonga uhuru wa vyombo vya habari.

Mwandishi ni Mkurugenzi Mkuu wa taasisi ya utafiti ya Twaweza.